

## NOVENA YA MOYO MTAKATIFU WA YESU

### SALA MWANZO;

Sala ya kutubu ikifuatiwa na sala au wimbo wa kumwalika Roho Mtakatifu.

1.Ee Yesu uliyesema” Kweli nawaambieni, ombeni nanyi mtapewa, tafuteni nanyi mtapata, gongeni nanyi mtafunguliwa” tazama ninagonga, ninatafuta na kuomba.....

Baba Yetu.....

Salaam Maria....

Atukuzwe Baba.....

Moyo Ntakatifu wa Yesu, ninakutumainia kwa moyo wangu wote.

2. Ee Yesu uliyesema “Kweli nawaambieni, chochote mtakachomwomba Baba kwa jina langu mtapewa”, tazama kwa jina lako ninaomba.....

Baba Yetu.....

Salaam Maria....

Atukuzwe Baba.....

Moyo Mtakatifu wa Yesu, ninakutumainia kwa moyo wangu wote.

3. Ee Yesu uliyesema “Kweli nawaambieni mbingu na dunia zitapita lakini maneno yangu hayatapita kamwe”. Tazama nikiwa nguvu na maneno yako ya kweli , ninaomba.....

Baba Yetu.....

Salaam Maria....

Atukuzwe Baba.....

Moyo Ntakatifu wa Yesu, ninakutumainia kwa moyo wangu wote.

Ee Moyo Mtakatifu wa Yesu, ambaye kwako ni kitu kimoja tu kisichowezezana, ambacho ni kutoacha kuwaonea huruma wenye huzuni, utuhurumie sisi wakosefu maskini na utujalie neema tukuombayo kwa njia ya Moyo Immakulata wa Maria, Mama yetu Mpole,

Sali 'Salamu Malkia'..... na kuongezea. Mt. Yosefu Baba Mlishi wa Yesu , utuombee.

Ongeza Rozari ya Moyo Mtakatifu wa Yesu na Litanja yake.....

**MWISHO:WIMBO WA MOYO MTAKATIFU WA YESU.**

**MOYO MTUKUFU WA MWOKOZI**

*Kiit:Moyo mtukufu wa Mwokozi ndipo nakimbiliapo,*

*Ukachomwa ukae wazi (ni salama niingiapo)x2*

1. Mfalme wangu yupo mbinguni, ndiye Yesu Bwana wangu,nafurahi, heshima gani kwani ni mtoto wa Mungu.
2. Shetani hana nguvu nami hai pati roho yangu, meno yake hayaniumi, kwani ni mtoto wa Mungu.
3. Dhoruba zikivuma kali, wakitetema wenzangu, miye ni mtulivu, nasali, kwani ni mtoto wa Mungu.
4. Nikiwa na magonjwa , taabu moyo hujazwa machungu, nashukuru kwa majaribu kwani ni mtoto wa Mungu.
5. Daima namfuata Bwana, na sauti yake Bwana, ninamrukia kama ndege kwani ni mtoto wa Mungu.

Moyo Mt. wa Yesu x3.....

Tunakimbilioa Ulinzi wako.....

***Ave Maria!***

***Mapendo ni ya Milele! (“.....imewapasa kumwomba Mungu siku zote...”)(Lk. 18:1)***